



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA



## TANZIA



Mstahiki Meya wa Jiji la Tanga, Mhe. Al-Hajj Abdulrahman O. Shiloow, anasikitika kutangaza kifo cha **Mheshimiwa LONGSON DAVID NJAU**, aliyekuwa Diwani wa Kata ya Masiwani, kilichotokea usiku wa kuamkia leo, Jumatano, Septemba 18, 2024, wakati akipokea matibabu baada ya kufikishwa Hospital jana usiku.

*“Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwa Mwenyezi Mungu tutarejea. Nimeshtushwa na nimesikitishwa sana na kifo cha Mhe. Njau. Mheshimiwa Njau alikuwa mtu mpole, msikivu, msomi, mchapakazi na mpenda maendeleo. Mara nyingi ametoa mawazo na ushauri wake kwenye vikao ambao umeleta mchango mkubwa katika maendeleo ya Jiji letu.”* Amesema Mstahiki Meya Shiloow.

Mstahiki Meya ametoa pole kwa wafiwa wote, wakiwemo familia ya marehemu, Waheshimiwa Madiwani, Wakazi wa Kata ya Masiwani, ndugu, jamaa na marafiki. Taarifa zaidi juu ya taratibu za msiba zitatolewa baada ya kikao na ndugu wa marehemu.

Mussa Labani.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini.